. TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Maonyesho ya “Swahili Fashion Week & Awards” kwa mwaka wa 2021 yamezinduliwa rasmi.

Maonyesho hayo ambayo ya 14 ya “Swahili Fashion Week” yanatarajiwa kufanyika Desemba 3, 4 & 5, mwaka huu katika Hoteli ya Serena jijini Dar es Salaam.

Jumla ya wabunifu sitini (60) wataonyesha vipaji vyao katika jukwaa hilo jijini Dar es Salaam.

Swahili Fashion Week inaungana na serikali kusherehekea miaka 60 ya Uhuru.

Jukwaa kubwa la maonyesho ya mavazi Afrika la ‘Swahili Fashion Week & Awards’ (#SFW2021) limepanga kufanya maonyesho yake Desemba 3, 4 & 5 mwaka huu, katika Hoteli ya Serena jijini Dar es Salaam.

Linatarajia kuleta pamoja wabunifu wapatao 60 kutoka nchi za Afrika Mashariki na kwingineko ulimwenguni. Likiwa limejijengea mafanikio makubwa kwenye maonyesho yake miaka iliyopita, jukwaa la “Swahili Fashion Week & awards” bado linaongoza kwa umahiri katika tasnia hii ya ubunifu wa mavazi.

Muasisi wa “Swahili Fashion Week & awards” Mustafa Hassanali ana matumaini ya kuimarisha msingi wa ubora wa jukwaa hilo na kwa shauku kubwa anasema, “Lengo la kuendeleza tasnia ya ubunifu Afrika bado linabaki kuwa kipaumbele, kupitia jukwaa hili na mtandao wake mkubwa wa vyombo vya habari, watumiaji wa bidhaa za ubunifu wa Tanzania, Afrika na ulimwengu kwa ujumla sasa wataona mbadala wa bidhaa zinazoingizwa kutoka nje.

“Wakati wote tumekua tukitilia mkazo thamani ya bidhaa za ubunifu za Afrika kwa kuhamasisha dhana ya “Made in Africa” na kutengeneza bidhaa zenye hadhi ya kimataifa kwa misingi ya Kiafrika.”

Maonyesho haya ya kumi na nne (14) ya “Swahili Fashion Week & Awards” yataendelea kuwa kioo kwa maonyesho mengine ya mavazi Afrika kwa wabunifu wa Kitanzania, ukanda wa Afrika Mashariki hata wale wa kimataifa kwa mvuto na mandhari yake ya kipekee inayoendana na kauli mbiu ya jukwaa ya Tambua Kinachoipendezesha Afrika “Discover What Makes Africa Beautiful.”

“Tunauhamasisha umma wa Watanzania kupenda kuvaa mavazi yaliyobuniwa na wabunifu wa hapa Tanzania (Made in Tanzania). Kwa kufanya hivyo tunakuza vipaji vyao na kuwafanya siku moja kutambulika kama wabunifu wakubwa ulimwenguni. Upendo unaanzia nyumbani na ndiyo dhumuni la kufanya haya..kukuza tasnia hii ya ubunifu” amesema Benedit Msofe Mratibu wa Swahili Fashion.

Swahili Fashion Week inashirikiana na serikali na wananchi kusherekea miaka 60 ya uhuru wa Tanzania ikiwa na dhamira ya kuonyesha ubunifu wa kupendeza, ubora na uzuri wa nchi, ili kuitangaza na kuongeza uchumi.

Jukwaa pia linawahimiza wabunifu wachanga kutumia jukwaa hili, ikiwa ni hatua moja wapo katika kukuza vipaji vyao vya ubunifu. Kwa mara nyingine kutakua na shindano la wabunifu chipukizi linalojulikana kama “Washington Benbella Emerging Designers Competition” ambapo wabunifu 10 wanatarajiwa kuonyesha umahiri wao kwenye ubunifu kupitia jukwaa hili.

Katika Maonyesho ya mwaka huu pamoja na maonyesho ya mavazi (runway) yatakayofanyika kila siku kwa kipindi cha siku tatu mfululizo kuanzia saa 2.30 usiku, kutakua na Bazaar ambapo wabunifu wataonyesha na kuuza bidhaa zao mbalimbali kuanzia saa 1.00 usiku.

Sambamba na hilo tutasherehekea na kutambua mchango wa wadau mbalimbali kwenye tasnia ya ubunifu ambapo tuzo kutoka vipengele 26 zitatolewa.

Swahili Fashion Week Inaandaliwa na kuratibiwa na 361 Degrees Africa Ltd,

wenyeji wakiwa ni Hoteli ya Serena Dar es Salaam na inadhaminiwa na Ubalozi wa Italia Tanzania, Desperado, GIZ, Tanzania Women Chamber of Commerce (TWCC), Hugo Domingo, Image Masters, Asila's Make Up, Nexia SJ, Epidor, Events lites, Advertising Dar, Maasai Watchers, Spik N' Span, Khimji's, African Star, Kuambiana Investment Company, A1 Outdoor, Fashion Association of Tanzania pamoja na Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA).

Wabunifu watakao onyesha ubunifu wao katika jukwaa hili kutoka mataifa mbalimbali ni;

Ashubira Designs (USA), Berry Heart Creations (Botswana), Clavon Leonard (USA), Dapperluq Collection (USA), Dimass Fashion Designs (Zambia), Endelea (Italy + Tanzania), Eisul Limited (Kenya), Jonjo Fashions (Uganda), KA Haute Kouture (Rwanda), ManeMane (Spain), Mshona (Uganda), NgapX (Namibia), PriscieB (Uganda), Sir Pinto's Design (Uganda), SixFit Unltd Wear (Uganda) and Ucoco Brand (Burundi) na pia tunatazamia kuwepo kwa wabunifu from Oman, Italy and Swedens siku za karibuni tutawatambulisha.

Kutoka Tanzania ni:

Affrican Attire For All (DSM), Africantouch Fashion Brand (DSM), AngelHudson (DSM), Bahati (ZNZ), Bhuyeg'I (DSM), Bilan Facon (DSM), Chuwa Fashion (Arusha), DD_Crafts (ZNZ), Difa_Designs (DSM), Doreen Mashika (ZNZ), Drax Fashion (DSM), EK-AN-TIK (DSM), Enofits (DSM), Getrude Shoo (Arusha), indigenous.I. (DSM), JK Design (DSM), Julia By Don Bosco (DSM), Kanyali Fabrics And Design (DSM), Kasikana Collection (Geita), Katty Collection (DSM), Kemi Kalikawe Ready To Wear (DSM), Kiki's Fashion (DSM), Levra With Culture (DSM), Lundi & Sons (DSM), Mahaumes Designs (DSM), MDC (DSM), MK Nuru Designs (DSM), Mkwanduleson's (DSM), Moshaki By Florence (DSM), Neah Collection (Tanga), Neith Design (Arusha), Neste Fashions Africa (DSM), Nyuzi CAD (DSM), Posh By Rinkie (DSM), Romy Jay (DSM), Scorpion Fashion And Style (DSM), Sukaina Kermali Apparel (DSM), WEEDO Women Empowering (DSM) and Zuh Fashion (DSM).

Kuhusu Swahili Fashion Week:

Swahili Fashion Week ni Jukwaa kubwa la maonyesho ya mavazi Afrika Mashariki na Kati linalotoa fursa kwa wabunifu wa mavazi kutoka nchi zinazozungumza lugha ya Kiswahili na kwingineko Afrika kuonesha vipaji vyao na kupanua wigo wao wa masoko.

Dhamira kuu ni kudhihirisha kwamba ubunifu wa mavazi ni shughuli inayoweza kumwingizia mtu kipato sambamba na kuhamamisha dhana ya Made in Africa.

Maonyesho ya Swahili Fashion Week yalianzishwa mwaka 2008 na muasisi wake Mustafa Hassanali.

Mwaka huu wa 2021 ni mara ya 14 yanafanyika tangu kuanzishwa kwake.

Swahili Fashion Week & Awards

Tembelea tovuti yetu : www.swahilifashionweek.com

Barua pepe: info@swahilifashionweek.com

Instagram @swahilifashionweek

Facebook @Swahilifashionweek

Twitter/snapchat/tiktok @swahilifashion

hashtag #sfw2021.